



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 26 Mei, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2022/2023.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2022/2023.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

133. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ni hatua nzuri ya dharura ya kuwahamisha wafanyabiashara wa soko la Mwanakwerekwe na kuwatengea eneo la muda maeneo ya Mwanakwerekwe "C". Hata hivyo, inasikitisha kuona kwamba kumekuwa na makusanyo ya maegesho katika sehemu isiyo rasmi ikiwemo maeneo ya hifadhi ya barabara (road reserves)

na malipo mengi yakifanyika bila risiti.

- (a) Je, Serikali imeridhia kuzigeuza hifadhi za barabara (road reserves) kuwa maegesho.
- (b) Je, Serikali haioni ulazima wa kuhamasisha biashara katika masoko kwa kuwa na utaratibu wa kutowalipisha ada ya maegesho wananchi wanaoenda sokoni kibiashara.
- (c) Je, ni ipi bei elekezi ya maegesho katika hifadhi ya barabara (road reserves) kwa magari vespa, pikipiki na baiskeli.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

124. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kimataifa inatambulika kwamba ufanisi katika operesheni za bandari unategemea moja kwa moja na uwepo wa vifaa vya kutosha vinavyokidhi kazi za kuteremshia na kuhifadhia mizigo yakiwemo makontena. Hata hivyo, tatizo la ukosefu na upungufu wa vifaa vinavyokidhi na kuhimili shughuli za Bandari ya Zanzibar limekuwa la muda mrefu pamoja na ukweli kwamba bajeti hutengwa mwaka hadi mwaka.

- (a) Je, Serikali imeshindwa kuzipatia ufumbuzi changamoto za operesheni za bandari.
- (b) Je, ni asilimia ngapi ya vifaa vimekosekana na asilimia ngapi ya ufanisi wa operesheni za Bandari ya Zanzibar unakosekana kwa sasa.
- (c) Je, ni hatua zifi za dharura na zifi za kudumu Serikali inazichukua ili kutatua tatizo la ufanisi mdogo wa Bandari ya Zanzibar unaosababishwa na ukosefu au uhaba wa vifaa vya kuteremshia au/na kuhifadhia mizigo.

180. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

- (a) Je, Wizara haitambui athari za mionzi inayotokana na uwepo wa minara ya simu karibu na makaazi ya watu na ni zifi hizo athari.

- (b) Je, ni fidia gani wananchi wanapata ukitoa mmiliki wa kiwanja anaefaidika moja kwa moja.

Wizara ya Afya:

103. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kuimarisha huduma bora kwa wananchi wake hasa huduma za afya. Hata hivyo ipo changamoto ya umbali wa huduma hiyo kwa wananchi wa shehia ya Kinowe kutokana na kutokuwepo kwa kituo cha afya katika shehia hiyo.

- (a) Je, Serikali kupitia Wizara yako inalijua tatizo hilo.
- (b) Kama inalijua, Je, Wizara ina mpango gani wa kuwatatulia wananchi hao tatizo hilo.

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

132. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kumekuwa na jitihada kubwa za Serikali katika kutumia rasilimali za bahari ili kujenga uchumi imara. Hata hivyo, hakujaonekana jitihada muafaka katika kuzitumia rasilimali zilizoko chini ya bahari (seabed) ambazo katika nchi nyingi zenyet rasilimali ya bahari zimekuwa zikileta mchango mkubwa katika uchumi wa nchi husika.

- (a) Je, Serikali imefanya utafiti wowote kutambua uwepo wa rasilimali za chini ya bahari (seabed) ya Zanzibar.
- (b) Je, Zanzibar ina ukubwa gani wa rasilimali ya chini ya bahari (seabed) na katika maeneo gani.
- (c) Je, ni madini ya aina gani yako katika eneo la chini ya bahari (seabed) ya Zanzibar.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

149. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

- (a) Ni tafiti zipi mpaka sasa zimefanywa na wataalamu wa kilimo wazawa ambazo zimeleta matokeo chanya.
- (b) Je, ni taasisi zipi binafsi zinazotoa misaada na mikopo nafuu kwa wakulima wetu.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
26 Mei, 2022.



(Raya Issa Msellel)
KATIBU WA BARAZA